BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA NANE</u>

<u>Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 26 Februari, 2025.</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:</u>

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

## II. <u>MASWALI:</u>

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

109. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni kwa kiasi gani Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kinasimamia vyema suala zima la ulinzi kupitia bahari zetu.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

104. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Utaratibu uko vipi juu ya muda wa kumaliza mashauri ya kesi za madai na kesi za jinai.

148. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali imeanzisha mfumo mzuri wa Zan Ajira ambao waombaji kazi katika sekta ya umma wanautumia.

Je, ni kwa kiasi gani mfumo mpya wa ajira Zan Ajira unasaidia katika kupambana na rushwa, uwajibikaji na utawala bora katika suala zima la vijana kunufaika na fursa za ajira.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

61. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Pamoja na Idara ya Usalama na Afya Kazini (OSHA) kuwa ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, bado Idara hii inaonekana kutofanya kazi kwa ufanisi, kiasi ya kuipelekea Serikali kukosa mapato mengi kutokana na sheria zilizopitwa na wakati na ukosefu wa mamlaka kwa Idara hiyo.

(a) Je, ni lini Serikali italeta sheria katika Baraza la Wawakilishi ili kuifanya OSHA kuwa na mamlaka kamili.

(b) Je, Serikali hupata kiasi gani cha mapato kwa mwaka kutokana na malipo ya huduma zinazotolewa na OSHA.

(c) Je, ni vikwazo vipi vinavyofanya OSHA kushindwa kuwa mamlaka inayoweza kusaidia nchi katika maendeleo.

111. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Miongoni mwa ahadi zako Mheshimiwa Waziri wakati tunapitisha bajeti ya Wizara yako ni kutembelea Chuo cha Ujasiriamali kilichopo Mwanakwerekwe.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri utafanya ziara hiyo inayosubiriwa kwa hamu na vijana hao.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi :**

167. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ukiachilia mbali fursa ya uvuvi wa samaki, bahari ni makazi ya asilimia 80 ya majani ya wanyama kama chanzo kikuu cha kujipatia riziki.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatoa hamasa, elimu na miongozo kwa wananchi kuzitambua fursa lukuki za matumizi ya bahari.

(b) Wizara inalichukulia vipi kwa umakini suala la usawa wa kijinsia katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi.

(c) Kwa kiasi gani na vipi watu wenye mahitaji maalum wanakuwa nao ni wanufaika wa fursa lukuki za uchumi wa buluu.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

17. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zanzibar ni moja ya maeneo yanayopaswa kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Wanyama wanaohama kutoka sehemu moja hadi nyingine (Conservation of Migratory Species).

(a) Je, Zanzibar inatekeleza vipi mkataba huu muhimu wa wanyama wenye tabia ya kuhama.

(b) Je, sheria na kanuni zetu za uhifadhi zinachangia kwa kiasi gani katika kulinda mkataba huu muhimu kwa wanyama.

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Kitathmini kwa kiasi gani kilimo chetu bado kinategemea mvua na kuwa cha msimu.

(b) Uwiano uko vipi juu ya kilimo cha msimu kinachotegemea mvua na matarajio ya kuvuka kuelekea kwenye kilimo cha umwagiliaji maji kwa kiwango cha kuridhisha.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

122. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mziki wa taarabu asilia umekuwa na wadau pamoja na wapenzi wengi nchi za Ulaya kama vile Belgium, Spain, Uingereza na nyenginezo.

Ni ipi mipango ya Wizara yako ya kuvifungulia fursa vikundi vya taarabu asilia kuupiga mziki huu nje ya nchi.

126. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kuna jitihada zipi za Wizara yako za kuiboresha michezo na kuipaisha ligi kuu ya Zanzibar katika viwango bora vinavyotambulika.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, kwa kiasi gani suala la uwepo wa wataalamu wa masuala ya ustawi wa jamii katika skuli zetu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum, linazingatiwa kwa unyeti wake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

177. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ilielezwa kwamba barabara ya Kiungoni -Tovuni ilikuwa ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa tuta la kuzuia maji chumvi la Tovuni katika jimbo la Pandani. Hata hivyo, pamoja na kuanza kwa hatua za awali, hadi sasa barabara ya Kiungoni - Tovuni haijajengwa.

(a) Je, ni lini barabara ya Kiungoni -Tovuni imepangwa kukamilishwa.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba mzunguko wa barabara ya Kiungoni kupitia Skuli ya Msingi Kiungoni inakuwa sehemu ya mradi huo na lini ujenzi unatarajiwa kuanza.

187. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na miradi mingi ya Serikali ambayo gharama zake hubadilika kwa kuongezeka sana wakati wa utekelezaji kutoka gharama ya awali ya mkataba.

(a) Je, ni gharama za kiasi gani zimekisiwa kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

(b) Je, uwanja huo mpya una mawanda ya kiasi gani ukilinganisha na mawanda ya Uwanja wa Kimataifa wa Msalato wa Dodoma.

(c) Je, ni ipi ratiba mpya ya utekelezaji wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

43. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kiasi gani kukuwa na kuimarika kwa miradi mbali mbali ya sekta za afya nchini, kunawapa fursa wafanyabiashara wa ndani kunufaika na uwepo wa miradi hii.

44. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Wajasiriamali wengi nchini wamekuwa wakipata changamoto ya gharama za kununua vifungashio.

Kwa kiasi gani Serikali inalifuatilia na kulipatia ufumbuzi tatizo hili.

**Wizara ya Afya:**

143. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na dhana kuwa wakati wa mabadiliko ya hali ya hewa hujitokeza magonjwa mbali mbali yanayoiathiri jamii.

(a) Je, ni aina gani ya magonjwa ambayo yanatokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

(b) Je, ni kwa kiasi gani Wizara inayadhibiti na inaelimisha jamii juu ya kuchukua tahadhari pindi tu yanapotokezea magonjwa hayo.

180. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kifungu cha 2 cha Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar ya mwaka 2023 imeyatambua makundi sita (a - f) yatakayosajiliwa na kuhudumiwa na Mfuko. Hata hivyo, pamoja na udogo wa Zanzibar, mchakato wa kuwasajili wanufaika umekuwa wa kasi ndogo na isiyoridhisha.

(a) Je, hadi hivi sasa, ni makundi mangapi kati ya sita tayari yameshasajiliwa na yanapata huduma za ZHSF.

(b) Je, ni ipi hadhi ya utambuzi wa wategemezi na wenza wa wachangiaji.

(c) Je, ni changamoto zipi zimejitokeza katika utaratibu wa kuhama waliokuwa wanachama wa NHIF kuingizwa katika mpango wa ZHSF.

## III. <u>TAARIFA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Zanzibar,**
**26 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**